# *Upelelezi wa Mauaji (Kutambua Watu) Sheria ya mwaka 2002 (CIIPA)*

Mwezi Novemba 2013, Serikali ya Australia ya Magharibi ilipitisha ***Upelelezi wa Mauaji (Kutambua Watu) Sheria iliyobadilishwa ya 2013 (CIIPA)***. Nguvu mpya imeingizwa ndani ya kifungu cha 16 ya CIIPA. Madhumuni ya nguvu mpya katika CIIPA ni kuwawezesha Maafisa wa Polisi kumtaka mtu kuondoa kifuniko cha uso au kufanya jambo jingine lolote muhimu ili kuwawezesha Ofisa wa Polisi kuweza kuona uso wa mtu kwa lengo la kumtambua.

Vyombo vya habari vimelenga katika marekebisho haya ya kisheria kama vile 'Sheria ya Burqa' wakati Polisi ya Australia ya Magharibi ikipitia upya nguvu za kutambua watu baada ya tukio lililotangazwa sana lililoshirikisha mwanamke aliyevaa Burqa katika New South Wales. Ilibainika kuwa kulikuwa na baadhi ya hali na mapungufu katika sheria ya Australia ya Magharibi ambayo ilipunguza uwezo wa polisi kutambua vizuri watu.

Huo upungufu umeweza kushughulikiwa na mabadiliko hayo ya sheria.

## Sheria

Kifungu cha 16 (4 A) CIIPA hutoa nguvu kwa polisi kuweza kuomba kuondolewa au kufanya marekebisho kitu kilichofunika uso kuvuliwa na mtu, au kuomba mtu kufanya chochote ambacho ni busara ili kuwawezesha afisa kuona uso wa mtu au kuthibitisha usahihi wa habari za mtu zilizotolewa

## Ufafanuzi

Kufunika uso ina ufafanuzi mpana sana na inajumuisha pamoja na kitu chochote kinachovaliwa na mtu ambacho kinafuniko sehemu ya uso au uso wote wa mtu. Mifano ni pamoja na kofia, helmeti, na miwani au maski za uso. Inaweza kujumuisha mtu ambaye amevaa rangi ya usoni au mapambo ambayo yanabadilisha muonekano wa mtu au unaficha kutambua hulka ya uso wa mtu

# MASWALI

## Ni wakati gani polisi wanaweza kunitaka niondoe kifuniko cha uso ?

Kipengere cha 16 cha *Upelelezi wa Mauaji (Kutambua Watu) Sheria ya mwaka 2002 (CIIPA)* kinaruhusu ofisa wa polisi kuweza kuomba habari za mtu binafsi na baadaye kuomba kuona uso wake, kama ofisa ana sababu za kuhisia:

- mtu huyo ametenda, anatenda au anakaribia kutenda kosa; au
- mtu huyo anaweza kusaidia katika upelelezi wa makosa au kosa linaloweza kutokea.

Katika hali ya vitendo, Maafisa wataweza kuhitaji marekebisho au kuondolewa kwa kifunika cha uso hata kama ombi hilo linahusiana na kosa kubwa au dogo ikiwa ni pamoja pale mtu anapopewa wito au ukiukwaji kwa makosa madogo ya barabarani kama vile kuendesha kwa mwendo kasi.

## Nina wajibu gani wakati nikitakiwa kuondoa kitu kilichofunika uso?

Unatakiwa kuondoa au kurekebisha uso uliofunikwa ili kusaidia Ofisa wa Polisi katika kukutambua wewe. Hiyo inaweza kuhusisha kuondoa au kurekebisha sehemu kubwa au ndogo inayofunika uso wako.

Ofisa wa Polisi atakutaka wewe tu kuondoa au kurekebisha uso uliofunikwa kwa kiasi kinachotoshereza kutambua wewe. Hii inaweza kujumuisha, kama inavyoweza kuonekana na kupata uhalali wa hati ya utambulisho kama vile Leseni ya dereva au Pasipoti.

Unatakiwa pia kusubiri katika kundi la afisa wa polisi mpaka wakati kama vile utakapokuwa umetimiza matakwa na afisa ameweza kuthibitisha usahihi wa maelezo yoyote binafsi uliyoyatoa.

## Inakuwaje kama naonekana tofauti na Leseni yangu au picha ya Pasipoti? Je, Polisi watanitaka kuondoa au kurekebisha kifuniko cha uso ili tu kulinganisha Leseni ya dereva wangu au picha ya Pasipoti?

Kama wakati huo, Polisi wakihitaji uondoe au kurekebisha kifuniko cha uso ili kukutambua, basi Polisi watakutaka ufanye hivyo. Picha katika leseni ya dereva au pasipoti zinaweza kusaidia polisi katika kukutambua

## Je naweza kuomba mtu wa jinsia moja na yangu kuwepo tu wakati naondoa kifuniko cha uso?

Sera ya polisi itahitaji maafisa kukumudu wewe kwa kiasi kizuri cha faragha na kama kuna afisa wa jinsia sawa na yako, afisa huyo atalazimika kufanya huo utambulisho

Kwa sababu za kiutendaji na kikazi inaweza kuwa vigumu kutaka polisi wa kike kuhudhuria katika kila tukio.

## Je, inakuwaje kama afisa wa jinsi sawa hayupo, je bado nahitajika kufuata matakwa yao?

Ndiyo, unalazimika kuzingatia ombi, lakini sera ya polisi inamtaka afisa kuchukua hatua zote nzuri katika kuheshimu utu wako na faragha labda kama kuna haja ya sababu za kiusalama, utaratibu wa kukutambua utafanyika mbele ya polisi mmoja.

## Inakuwaje kuhusu usiri wangu?

Ofisa wa Polisi anayefanya ombi la kukukagua atatumia hali ya juu ya faragha katika mazingira husika. Kama inawezekana, Maafisa wa Polisi wanaweza kukubaliwa kukukagua kwa faragha ya ziada kwa mfano kwa kuhudhurio katika kituo cha Polisi kwa ajiri ya kurekebisha au kufunua uso wako.

Hata hivyo, kama ombi lako la kutaka faragha haliwezi kuzingatiwa katika mazingira hayo, unalazimika bado kuzingatia ombi la Ofisa wa Polisi.

Sera ya Polisi inasema kuwa wakati wa kushughulika na watu ambao wamevaa vifuniko vya uso kwa sababu za kitamaduni au kidini, Maafisa wa Polisi lazima kuhakikisha kuwa wanafanya kwa kuzingatia usiri unaoendana na imani ya mtu.

## Je inakuwaje kama nikishidwa kufuata matakwa?

Ni kosa kukataa kuondoa au kurekebisha uso wako uliofunikwa wakati ukiombwa na afisa wa polisi. Kukataa kuzingatia inaweza kusababisha wewe kukamatwa na kushtakiwa.

Kushindwa kuzingatia sheria hiyo huchukua kiwango cha juu cha adhabu  ya miezi 12 jela.

## Je naweza kuomba Ofisa wa Polisi kuelezea hili zaidi?

Ndiyo, unaweza kuomba Ofisa wa Polisi kueleza ombi lake kwa ajili ya marekebisho au kuondolewa kwa kifuniko usoni. Kama kawaida, Maafisa wa Polisi watalazimika kueleza ombi hilo.

Kama unapata ugumu katika kuelewa Kiingereza, mkalimani anaweza kutafutwa ili kusaidia afisa kuridhika kwamba umeelewa nini unatakiwa kufanya na kwa nini umetakiwa kufanya hivyo.